**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

# MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2026/27

**MACHI 2026**

# YALIYOMO

**1.0. UTANGULIZI ... 3**
**2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2024/25 ... 4**
**3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2025/26 ... 5**
**3.1. Mapitio ya Shabaha na Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2025/26 ... 5**
**3.2. Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2025/26 ... 6**
**3.3. Utekelezaji wa Bajeti kwa Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2025/26 ... 6**
3.3.1. Mapato ... 6
3.3.2. Matumizi ... 7
3.3.1. Kugharamia Nakisi ... 7
3.3.2. Mafanikio Katika Utekelezaji wa Bajeti ... 7
3.3.3. Changamoto Katika Utekelezaji wa Bajeti ... 8
3.3.4. Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Zilizojitokeza ... 8
3.3.5. Mwenendo wa Deni la Serikali ... 10
**4.0. MAPENDEKEZO YA MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 2026/27 ... 11**
**4.1. Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla na Bajeti ... 11**
**4.2. Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato ... 11**
**4.3. Sera na Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi ... 12**
**4.4. Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2026/27 ... 13**
(i) Kujenga Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani Utakaotekelezwa Kupitia Sekta Tisa (9) za Mageuzi ... 13
(ii) Kuimarisha Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii ... 14
(iii) Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ... 14
(iv) Vichocheo vya Mageuzi ... 14
(v) Utawala, Amani, Usalama na Utulivu ... 15
**4.5. Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/27 ... 15**
**4.6. Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti ... 18**
4.6.1. Vihatarishi vya Uchumi Jumla ... 18
4.6.2. Vihatarishi Mahsusi ... 19
**5.0. HITIMISHO ... 22**

## 1.0. UTANGULIZI

1. Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27 imeandaliwa kwa mujibu wa Ibara ya 137(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 23 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439. Mfumo na ukomo wa bajeti unaopendekezwa ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV, 2026/27 – 2030/31). Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi; sehemu ya pili ni mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25; sehemu ya tatu ni mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/26; sehemu ya nne ni mapendekezo ya mfumo na ukomo wa bajeti ya mwaka 2026/27; na sehemu ya tano ni hitimisho.

2. Katika mwaka 2024/25, Serikali ilikusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 49,821.2 kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na asilimia 99.1 ya lengo la mwaka. Aidha, nakisi ya bajeti iliendelea kuimarika na kufikia asilimia 3.1 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2023/24 kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti.

3. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2025/26 ni shilingi bilioni 56,490.3. Hadi Desemba 2025, Serikali ilifanikiwa kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 28,215.4 kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na asilimia 100.2 ya lengo la kipindi hicho.

4. Mafanikio ya utekelezaji wa bajeti ni pamoja na: kulipa mishahara na deni la Serikali kwa wakati; kudhibiti mfumuko wa bei ndani ya wigo wa tarakimu moja; kugharamia Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025; kuendelea kugharamia miradi ya kimkakati ikiwemo umeme, SGR na mji wa Serikali Mtumba; kuongezeka kwa mapato ya kodi; na kugharamia huduma muhimu za kijamii ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii. Pamoja na mafanikio hayo, changamoto pia zilijitokeza ikiwemo: mabadiliko ya sera za washirika wa maendeleo; kutozingatiwa ipasavyo kwa vipaumbele wakati wa uandaaji na utekelezaji wa bajeti, hivyo kusababisha uhitaji mkubwa wa rasilimali fedha wakati wa utekelezaji na mahitaji makubwa ya uhamisho wa bajeti; na mwitikio mdogo wa matumizi ya teknolojia na miundombinu ya malipo bila fedha taslimu katika huduma. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato ikiwemo Mkakati wa Muda wa Kati wa Kuongeza Mapato ya Serikali (2025/26 – 2027/28), kufanya uhamisho wa bajeti kwa mahitaji ya msingi, kuwianisha mapato na matumizi, kuwezesha na kuimarisha sekta binafsi katika uibuaji, utekelezaji, uendeshaji wa miradi na utoaji wa huduma, na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika malipo, utoaji huduma na usimamizi wa fedha za umma.

5. Mapendekezo ya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27 yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo matano (5) ya vipaumbele yaliyoainishwa katika FYDP IV ambayo ni (i) kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani utaotekelezwa kupitia sekta tisa (9) za mageuzi (ii) kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii (iii) Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya

tabianchi (iv) vichocheo vya mageuzi na (v) Utawala, Amani, Usalama na Utulivu. Aidha, Serikali itaweka msukumo katika ukamilishaji wa miradi na programu za maendeleo zinazoendelea, kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi na kuwezesha Serikali kuwekeza katika miradi ya kimkakati itakayochochea ukuaji wa uchumi na ajira.

6. Katika mwaka 2026/27, Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 62,334.2, sawa na ongezeko la asilimia 10.3 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/26. Sehemu kubwa ya ongezeko hili itagharamia mishahara, malipo ya deni la Serikali, malimbikizo ya madai ya wakandarasi, michango ya Serikali katika mfuko wa pensheni, mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na fedha za Mifuko ambazo kwa pamoja zitatumia takribani asilimia 75 ya ongezeko la bajeti. Bajeti hiyo inatarajiwa kugharamiwa kutoka vyanzo vya ndani na nje ambapo mapato ya kodi ni shilingi bilioni 36,989.3, mapato yasiyo ya kodi shilingi bilioni 9,238.8 na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 563.1. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 15,542.9 kutoka vyanzo vya nje na ndani.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2024/25

7. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha bajeti ya Serikali ya shilingi bilioni 50,291.4 kwa mwaka 2024/25. Hadi Juni 2025, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 49,821.2 kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na asilimia 99.1 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, asilimia 70 ni mapato ya ndani shilingi bilioni 34,845.9, sawa na asilimia 100.7 ya lengo la mwaka na misaada shilingi bilioni 880.1 sawa asilimia 110.8. Mapato yanayokusanywa na TRA yalifikia shilingi bilioni 30,095.7 sawa na asilimia 102.3 ya lengo la mwaka. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 4,750.1 sawa na asilimia 91.4 ya lengo zikijumuisha: Maduhuli yanayokusanywa na MDAs ambayo yalifikia shilingi bilioni 3,312.9 sawa na asilimia 86.3 ya lengo na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo yalifikia shilingi 1,437.3 sawa asilimia 106.0 ya lengo. Aidha, mikopo ya ndani na nje ilikuwa shilingi bilioni 14,095.2 sawa na asilimia 94.7 ya lengo.

8. Katika mwaka 2024/25, Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 49,821.2, sawa na asilimia 99.1 ya bajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 34,418.4 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara ya watumishi wa umma, ugharamiaji wa deni la Serikali na uendeshaji wa shughuli za Serikali. Aidha, shilingi bilioni 15,402.7 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 12,715.9 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 2,686.8 ni fedha za nje**.** Nakisi ya bajeti iliendelea kuimarika na kufikia asilimia 3.1 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2023/24 kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti. **Jedwali Na. 1** limeainisha utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na. 1: Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2024/25** (shilingi milioni)

| | BAJETI | HALISI | UFANISI |
|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 34,610,646 | 34,845,867 | 100.7% |
| TRA | 29,415,289 | 30,095,736 | 102.3% |
| Mapato yasiyo ya kodi (MDAs) | 3,839,017 | 3,312,853 | 86.3% |
| Mapato ya Halmashauri | 1,356,341 | 1,437,278 | 106.0% |
| Misaada | 794,390 | 880,052 | 110.8% |
| Mikopo nafuu | 5,281,943 | 4,194,993 | 79.4% |
| Mikopo ya kibiashara nje | 2,986,638 | 2,410,774 | 80.7% |
| Mikopo ya kibiashara ndani | 6,617,790 | 7,489,466 | 113.2% |
| Kulipa mtaji | 4,022,373 | 4,087,193 | 101.6% |
| Kugharamia bajeti (NDF) | 2,595,417 | 3,402,273 | 131.1% |
| **JUMLA YA MAPATO** | **50,291,408** | **49,821,151** | **99.1%** |
| | | | |
| **JUMLA YA MATUMIZI** | **50,291,408** | **49,821,151** | **99.1%** |
| Matumizi ya kawaida | 34,937,808 | 34,418,429 | 98.5% |
| Mishahara | 11,767,987 | 11,238,563 | 95.5% |
| Deni la Serikali | 13,121,466 | 12,461,866 | 95.0% |
| Matumizi mengine | 10,048,356 | 10,718,000 | 106.7% |
| Matumizi ya maendeleo | 15,353,600 | 15,402,723 | 100.3% |
| Ndani | 11,712,762 | 12,715,894 | 108.6% |
| Nje | 3,640,838 | 2,686,829 | 73.8% |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2025/26

### 3.1. Mapitio ya Shabaha na Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2025/26

9. Katika bajeti ya mwaka 2025/26, Serikali ililenga kufikia malengo na shabaha za uchumi na bajeti ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

(i) **Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.5 mwaka 2024:** Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2025, ukuaji wa Pato la Taifa ulifikia wastani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, Sekta zilizokuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji katika kipindi cha marejeo ni pamoja na shughuli za uzalishaji umeme zilizokuwa na ukuaji wa asilimia 15.5, shughuli za fedha na bima (asilimia 14.8) pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 13.7). Shughuli za kilimo ziliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa jumla wa asilimia 6.0 ambapo ilichangia nukta za asilimia 0.9 katika ukuaji huo, ikifuatiwa na ujenzi pamoja na shughuli za uchimbaji madini na mawe zilizochangia nukta za asilimia 0.8, na fedha na bima nukta za asilimia 0.6.

(ii) **Kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha unabaki kwenye wigo wa wastani wa asilimia 3.0 hadi 5.0:** Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na

wastani wa asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa ugavi wa bidhaa za vyakula katika soko la ndani kufuatia ongezeko la mauzo kwenda nchi jirani. Pamoja na ongezeko hilo, kiwango cha mfumuko wa bei bado kipo ndani ya lengo la nchi.

(iii) **Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4):** Hadi Desemba 2025, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 6,329, ambapo kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.9. Ongezeko hilo lilichangiwa na utekelezaji thabiti wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu nchini, pamoja na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na mauzo ya dhahabu na korosho.

(iv) **Mapato ya ndani na mapato ya kodi kufikia asilimia 16.7 asilimia 13.3 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26, mtawalia; na kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa.** Tathmini ya malengo haya itafanyika mwishoni mwa mwaka wa fedha kufuatia kukamilika kwa takwimu halisi za Pato la Taifa. Aidha, kwa tathmini ya miezi sita ya mwanzo ya mwaka 2025/26 kwa mapato ya ndani, mapato ya kodi na viashiria vya Pato la Taifa, yameonesha mwenendo mzuri, hivyo malengo hayo yanatarajiwa kufikiwa kama ilivyokusudiwa.

### 3.2. Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2025/26

10. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2025/26 ni shilingi bilioni 56,490.3. Bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani shilingi bilioni 40,466.1 na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilioni bilioni 1,069.9. Aidha, nakisi ya bajeti inagharamiwa na mikopo ya ndani shilingi bilioni 6,278.2 na mikopo ya nje shilingi bilioni 8,676.1.

### 3.3. Utekelezaji wa Bajeti kwa Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2025/26

11. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, Serikali ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 28,215.4 kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na asilimia 100.2 ya lengo la kipindi hicho. Aidha, matumizi katika kipindi cha marejeo yalikuwa shilingi bilioni 28,215.4, sawa na asilimia 100.2 ya lengo.

#### 3.3.1. Mapato

12. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, mapato yalifikia shilingi bilioni 20,810.5, sawa na asilimia 98.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 21,027.7 katika kipindi hicho. Kati ya hayo, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 16,908.2, sawa na asilimia 103.0 ya lengo. Hii lilitokana na kuongezeka kwa kiwango cha uhiari wa kulipa kodi pamoja na kuongezeka kwa wigo wa vyanzo vya mapato ya kodi kufuatia kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Misaada ilikuwa shilingi bilioni 507.6, sawa asilimia 95.7 ya lengo na asilimia 1.8 ya mahitaji ya kipindi husika cha marejeo. Aidha, mapato mengine (mapato yasiyo ya kodi) yalikuwa shilingi bilioni 3,394.8 sawa na asilimia 83.0. Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kulitokana na: Kuwepo kwa mifumo isiyo na ufanisi katika ukusanyaji wa

mapato, jambo lililosababisha upotevu wa mapato yanayostahili kukusanywa kutoka katika chanzo hicho muhimu; Baadhi ya taasisi za umma na wakala wa Serikali zimeshindwa kuwasilisha kwa wakati, na kwa viwango vilivyokadiriwa, gawio na michango ya kisheria katika Mfuko Mkuu wa Serikali; na Kuendelea kwa vitendo vya magendo, hususan katika maeneo ya mipakani, kumeathiri ukusanyaji wa mapato yanayotokana na sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

### 3.3.2. Matumizi

13. Utekelezaji wa bajeti umeendelea kuzingatia maeneo ya vipaumbele ikiwa ni pamoja na ugharamiaji wa shughuli za uchaguzi mkuu, mahitaji ya sekta ya hifadhi ya jamii na ujenzi wa miundombinu ya nishati, usafiri na usafirishaji ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuimarisha ustawi wa jamii. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, jumla ya matumizi ya Serikali bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni ilikuwa shilingi bilioni 25,060.0, sawa na asilimia 100.8 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, mishahara na stahiki za watumishi ni shilingi bilioni 4,466.2 na malipo ya riba shilingi bilioni 2,952.4 na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi bilioni 1,776.2.

### 3.3.3. Kugharamia Nakisi

14. Serikali ilikopa ndani jumla ya shilingi bilioni 7,404.9 kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na asilimia 103.9 ya lengo. Aidha, Serikali ililipa mitaji iliyoiva jumla ya shilingi bilioni 3,155.37, na hivyo kufanya mikopo halisi kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti kuwa shilingi bilioni 4,249.5.

### 3.3.4. Mafanikio Katika Utekelezaji wa Bajeti

15. Mafanikio mbalimbali yamepatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025. Miongoni mwa mafanikio hayo ni:

(i) Kulipa mishahara ya watumishi na kugharamia deni la Serikali kwa wakati ambapo kiasi cha shilingi bilioni 9,704.3 kimetumika;

(ii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja wa asilimia 3.5 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025;

(iii) Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2025;

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kielelezo ikiwemo ujenzi wa SGR ambapo kiasi cha shilingi bilioni 630.4 kimetumika hadi Novemba 2025, miradi ya kuzalisha na kusambaza umeme shilingi bilioni 158.8 na uendelezaji wa mji wa Serikali Mtumba shilingi bilioni 225.8;

(v) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya kodi ambayo yalivuka lengo kwa asilimia 2.4 na yalikua kwa asilimia 19.1 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024/25.

(vi) Kuendelea kugharamia mahitaji ya sekta ya hifadhi ya jamii na huduma za jamii kwa wananchi ikiwemo mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya kati na elimu ya juu, elimu bila ada kwa shule za msingi na sekondari, dawa, vifaa na vifaa tiba, pamoja na usambazaji wa maji safi na salama ambapo jumla ya shilingi bilioni 8,973.5 zimetolewa kwa ajili ya sekta za huduma za jamii;

(vii) Kuandaa mashindano ya CHAN 2024 kwa kushirikiana na Kenya na Uganda ambayo yalifanyika Agosti 2025, ambapo Tanzania ilinufaika kwa kuongeza

fursa za ajira, kuimarika kwa mahusiano ya kidiplomasia pamoja na kukuza shughuli za utalii. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati mkubwa wa viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya michuano ya AFCON ya mwaka 2027 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 146.0 kimetumika; na

(viii) Kuendelea kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi wa umma, wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ambapo jumla ya shilingi bilioni 194.7 zimelipwa na hivyo kuendelea kuchachua shughuli za kiuchumi.

### 3.3.5. Changamoto Katika Utekelezaji wa Bajeti

16. Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2025 ni pamoja na:

(i) Kubadilika kwa sera za washirika wa maendeleo ambazo zimesababisha kupungua kwa misaada ambapo Umoja wa Ulaya umetangaza kuahirisha utoaji wa fedha za msaada kwa mikataba mipya ambayo Serikali ilitarajia kuingia yenye thamani ya takriban EUR milioni 156, sawa na shilingi bilioni 445.75. Kwa mikataba inayoendelea, Serikali inaweza kukosa misaada ya kibajeti kutoka Umoja wa Ulaya yenye thamani ya takriban EUR milioni 39.20, sawa na shilingi bilioni 113.8 kwa mwaka 2025/26;

(ii) Kutozingatiwa ipasavyo kwa vipaumbele wakati wa uandaaji na utekelezaji wa bajeti, hivyo kusababisha uhitaji mkubwa wa rasilimali fedha wakati wa utekelezaji wa bajeti na mahitaji makubwa ya uhamisho wa bajeti;

(iii) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi hasa ya ndani katika kuwekeza na kuendesha miradi ya maendeleo kutokana na upungufu wa mitaji; na

(iv) Mwitikio mdogo wa matumizi ya teknolojia na miundombinu ya malipo bila fedha taslimu katika huduma.

### 3.3.6. Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Zilizojitokeza

17. Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2026, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali itakayochochea ukuaji wa uchumi, kuongeza mapato na kuimarisha usimamizi wa matumizi ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza na hivyo kuwezesha kufikia shabaha na malengo ya Serikali kwa mwaka 2025/26. Mikakati hiyo ni pamoja na:

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Muda wa Kati wa Kuongeza Mapato ya Serikali (2025/26 – 2027/28) ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani;

(ii) Kuendelea na maboresho ya mifumo ya kukusanyia mapato yatokanayo na sekta ya utalii na ardhi ikiwa ni pamoja na kuifungamanisha na mifumo ya Uhamiaji, NIDA na mifumo ya usajili wa magari ya Serikali na magari ya nje ya nchi;

(iii) Serikali itaendelea kuwianisha mapato na matumizi huku ikihakikisha mahitaji ya msingi yanagharamiwa ikiwepo mishahara, deni la Serikali na huduma za jamii;

(iv) Kufanya uhamisho baina ya mafungu na ndani ya mafungu ili kumudu mahitaji ya msingi na yale ambayo hayakuwa sehemu ya bajeti ya mwaka 2025/26 iliyoidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa miongozo na taratibu zilizopo;

(v) Kuhamasisha ushirikishaji wa sekta zote husika wakati wa uandaaji wa

miradi inayohusisha sekta zaidi ya moja ili kurahisisha utekelezaji na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti;

(vi) Kuwezesha na kuimarisha sekta binafsi katika uibuaji, utekelezaji, uendeshaji wa miradi na utoaji wa huduma; na

(vii) Kuhamasisha na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika malipo, utoaji huduma, ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

18. Kipindi cha Januari hadi Juni 2026, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi shilingi bilioni 28,274.9 sawa na asilimia 50.1 ya bajeti ya mwaka 2025/26 ya shilingi bilioni 56,490.3. Kati ya kiasi kitakachokusanywa, mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 20,163.2, misaada shilingi bilioni 448.5 na mikopo ya ndani na nje shilingi bilioni 7,663.2. Mwenendo na mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2**.

### Jedwali Na. 2: Mwenendo na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2025/26

*shilingi bilioni*

| | 2025/26 Bajeti Iliyoidhinishwa | 2025/26 Bajeti iliyorekebishwa | Julai - Desemba 2025 | | | Mwelekezo hadi Juni 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Makadirio | Halisi | Ufanisi | |
| **A: Mapato** | **41,536.02** | **41,422.22** | **21,027.7** | **20,810.5** | **99.0%** | **20,611.7** |
| Mapato ya kodi | 32,176.00 | 32,176.00 | 16,409.49 | 16,908.2 | 103.0% | 15,267.8 |
| Misaada/Michango | 1,069.88 | 956.09 | 530.38 | 507.6 | 95.7% | 448.5 |
| Mapato mengine | 8,290.13 | 8,290.13 | 4,087.81 | 3,394.8 | 83.0% | 4,895.3 |
| o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,680.51 | 1,680.51 | 820.10 | 774.0 | 94.4% | 906.5 |
| | | | | | | |
| **B: Matumizi** | **48,775.0** | **48,775.0** | **24,862.3** | **25,060.0** | **100.8%** | **23,715.0** |
| Mishahara na stahiki za watumishi | 7,711.9 | 7,711.9 | 4,351.1 | 4,466.2 | 102.6% | 3,245.6 |
| Gharama za bidhaa na huduma | 7,812.2 | 7,812.2 | 3,144.0 | 3,480.7 | 110.7% | 4,331.6 |
| Malipo ya riba | 6,493.7 | 6,493.7 | 3,107.5 | 2,952.4 | 95.0% | 3,541.4 |
| Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji | 1,936.0 | 1,936.0 | 56.7 | 54.2 | 95.6% | 1,881.8 |
| Ruzuku na michango | 21,107.9 | 21,107.9 | 11,388.1 | 11,343.6 | 99.6% | 9,764.4 |
| Mafao na misaada ya kijamii | 752.5 | 752.5 | 249.4 | 233.5 | 93.7% | 519.0 |
| Gharama nyingine | 180.5 | 180.5 | 851.6 | 753.2 | 88.4% | (572.7) |
| Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha | 2,780.2 | 2,780.2 | 1,713.8 | 1,776.2 | 103.6% | 1,003.9 |
| | | | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti bila Misaada** | **(8,308.9)** | **(8,308.9)** | **(4,365.0)** | **(4,757.1)** | **109.0%** | **(3,551.8)** |
| | | | | | | |
| **Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada** | **(7,239.0)** | **(7,352.8)** | **(3,834.6)** | **(4,249.5)** | **110.8%** | **(3,103.3)** |
| | | | | | | |
| **Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti** | **7,239.0** | **7,352.8** | **3,834.6** | **4,249.5** | **110.8%** | **3,103.3** |
| **Mikopo Halisi** | **7,239.0** | **7,352.8** | **3,834.6** | **4,249.5** | **110.8%** | **3,103.3** |
| **D: Mikopo ya Ndani** | **2,952.6** | **2,214.1** | **1,323.9** | **1,725.5** | **130.3%** | **488.6** |
| D1 - Mikopo ya ndani | 6,278.2 | 5,539.7 | 2,616.3 | 3,017.9 | 115.4% | 2,521.8 |
| D2 - Malipo mikopo ya ndani | (3,325.6) | (3,325.6) | (1,292.4) | (1,292.4) | 100.0% | (2,033.2) |
| **D: Mikopo ya Nje** | **4,286.3** | **5,138.7** | **2,510.7** | **2,524.0** | **100.5%** | **2,614.7** |
| E1 - Mikopo ya nje | 8,676.1 | 9,528.4 | 4,513.2 | 4,387.0 | 97.2% | 5,141.4 |
| o/w Mikopo nafuu | 6,047.0 | 6,899.4 | 3,023.5 | 3,001.9 | 99.3% | 3,897.5 |
| o/w Mikopo ya Kibiashara | 2,629.0 | 2,629.0 | 1,489.7 | 1,385.1 | 93.0% | 1,243.9 |
| E2 - Malipo mikopo ya nje | (4,389.7) | (4,389.7) | (2,002.5) | (1,863.0) | 93.0% | (2,526.7) |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| **Jumla ya Bajeti Mapato ( A + D1 + E1)** | **56,490.3** | **56,490.3** | **28,157.1** | **28,215.4** | **100.2%** | **28,274.9** |
| | | | | | | |
| **Jumla ya Bajeti Matumizi (B - D2 - E2)** | **56,490.3** | **56,490.3** | **28,157.1** | **28,215.4** | **100.2%** | **28,274.9** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

### 3.3.7. Mwenendo wa Deni la Serikali

19. Hadi Desemba 2025, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 109,444.58 ikilinganishwa na shilingi bilioni 93,687.47 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.82 na asilimia 47 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 37,898.98 (sawa na asilimia 34.63 ya deni lote) na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 71,545.60. Ongezeko la deni limetokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji. Matokeo ya tathmini ya Uhimilivu wa Deni iliyofanyika Oktoba 2025 yalionesha kuwa deni limeendelea kuwa himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu.

20. Katika kuhakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:

(i) Kuhakikisha mikopo inayopewa kipaumbele ni ile yenye masharti nafuu kadri inavyopatikana. Mikopo yenye masharti ya kibiashara itaelekezwa katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi. Tathmini inaonesha kuwa deni la Serikali linaendelea kukua na moja ya sababu ikiwa ni kukopa bila kuwa na utayari wa kutekeleza miradi husika na

hivyo kupelekea kulipa gharama za kutunza mkopo (commitment fees). Hivyo ni muhimu kuhakikisha miradi iko tayari kwa utekelezaji ili kuepuka kulipa commitment fees.

(ii) Kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika bila kuathiri uendeshaji wa shughuli za Serikali;

(iii) Kusimamia utoaji wa dhamana kwa mashirika ya Umma. Hatua hii itasaidia kutokuongeza deni linalotokana na taasisi hizo kushindwa kulipa madeni; na

(iv) Kuendeleza mabadiliko ya kimuundo katika uchumi, na kutumia nafasi nzuri ya kijiografia ya nchi kuongeza mauzo ya nje na ushindani wa biashara ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

## 4.0. MAPENDEKEZO YA MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 2026/27

### 4.1. Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla na Bajeti

21. Shabaha na malengo ya uchumi jumla na bajeti ni kama ifuatavyo:

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2026;

(ii) Mfumuko wa bei kuwa kwenye wigo wa tarakimu moja wa kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27;

(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

(vi) Akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

22. Uandaaji shabaha za uchumi na bajeti kwa mwaka 2026/27 umezingatia misingi (*assumptions*) ifuatayo:

(i) Utekelezaji wa Mkakati wa Ukusanyaji Mapato wa Muda wa Kati (Medium Term Revenue Mobilization Strategy) 2025/26 – 2027/28;

(ii) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(iii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, tetemeko la ardhi, magonjwa ya mlipuko, mafuriko na migogoro ya kivita na kibiashara;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(v) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na

(vi) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

### 4.2. Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato

23. Katika mwaka 2026/27, Serikali itaendelea kuweka vipaumbele zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuongeza ufanisi na kupunguza utegemezi. Katika

kutimiza azma hiyo, Serikali itaweka msisitizo katika kutekeleza Mkakati wa Muda wa Kati wa Kuongeza Mapato ya Serikali (2025/26 - 2027/28). Maeneo muhimu ya mkakati ni pamoja na:

(i) Kuimarisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi kupitia huduma za elimu na uwezeshaji zitolewazo katika "Dawati la Kuwezesha Biashara" nchini;

(ii) Kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari nchini kwa kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na walipakodi kupitia majadiliano kwenye majukwaa mbalimbali ikiwemo Baraza la Taifa la Biashara na CEOs Round Table;

(iii) Kuendelea kusimamia na kuhimiza matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD) kupitia utoaji wa elimu na uendeshaji wa programu mbalimbali za hamasa;

(iv) Kuendelea kujenga na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha mifumo hiyo inaunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za umma kwa lengo la kupata taarifa za wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa katika mifumo na wale waliosajiliwa wanalipa mapato yao stahiki;

(v) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia za kibenki/kielektroniki kwenye kufanya malipo mbalimbali kupitia utoaji wa vivutio mbalimbali na ukusanyaji wa mapato;

(vi) Kuongeza kasi ya kupanga, kupima, kumilikisha na kurasimisha ardhi kwa kuweka msisitizo katika kutambua vipande vya ardhi nchini ili kuongeza wigo wa mapato;

(vii) Kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ikiwemo ufuatiliaji wa karibu wa mashirika ya umma ili kuhakikisha yanaongeza tija, gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati katika Mfuko Mkuu wa Serikali; na

(viii) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni ambao utachangia katika kuongeza mapato ya Serikali.

### 4.3. Sera na Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi

24. Katika mwaka 2026/27, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410. Lengo ni kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma ikiwemo kugharamia mahitaji yasiyoepukika kama mishahara na deni la Serikali pamoja na kuimarisha usimamizi wa miradi inayogharamiwa kwa fedha za mikopo ya nje. Mikakati mahususi ni pamoja na:

(i) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na matumizi ya mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuiunganisha ili iweze kubadilishana taarifa;

(ii) Kufanya upembuzi yakinifu na kujiridhisha na kuheshimu matakwa ya mikataba inayoingiwa na wawekezaji ili kuepuka gharama za kuvunja mikataba;

(iii) Utengaji wa fedha utazingatia mahitaji ya msingi yasiyoepukika (ikijumuisha mishahara na deni la Serikali), malimbikizo ya madai ya watumishi, wazabuni na wakandarasi, na ugharamiaji wa miradi ya

kipaumbele yenye kufungua fursa za kiuchumi kama ilivyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/27 ikiwemo ujenzi wa miundombinu wezeshi ya kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi;

(iv) Kutekeleza programu na miradi inayoendelea yenye matokeo ya haraka na inayojenga msingi wa mageuzi ya kiuchumi;

(v) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na utendaji kazi katika Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuboresha mikataba ya utendaji kazi, miundo ya taasisi na usimamizi wa bodi;

(vi) Kubainisha njia mbadala za ugharamiaji miradi (Alternative Project Financing) ikiwemo utaratibu wa PPP badala ya kutegemea bajeti kuu ya Serikali na kuimarisha na kuwezesha sekta binanfsi kupitia uandaaji wa miradi inayokopesheka (bankable projects);

(vii) Kufungamanisha utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo zenye malengo yanayofanana baina ya sekta ili kuongeza tija ya rasilimali za umma;

(viii) Kuendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaozingatia matokeo na uwajibikaji katika utendaji kazi wa Serikali na utekelezaji wa miradi; na

(ix) kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti, Sura 439, Kifungu 29 (1-2), kuwa Serikali haitaruhusu mafungu kuvuka na ridhaa za matumizi zisizokuwa na fedha mwisho wa mwaka 2025/26 na badala yake Mafungu yanaaswa kutenga bajeti ya miradi husika kwa mwaka 2026/27kwa kuzingatia vipaumbele na taratibu za bajeti.

## 4.4. Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2026/27

25. Bajeti ya mwaka 2026/27 ni ya kwanza katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kuifanya Tanzania kuwa Taifa Jumuishi, lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea ifikapo mwaka 2050. Dira hii inalenga kuifikisha Tanzania kwenye hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu, yenye Pato la Taifa la dola trilioni moja, kipato cha wastani wa angalau dola 7,000 kwa mtu, maisha bora kwa wote, uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, pamoja na jamii yenye ujuzi na matumizi ya teknolojia za kidijitali. Utekelezaji wa Dira 2050 utafanyika kupitia Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2050) na awamu tano za Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano, kuanzia FYDP IV ya mwaka 2026/27–2030/31.

26. Mapendekezo ya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27 yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo matano (5) ya vipaumbele yaliyoainishwa katika FYDP IV ambayo ni (i) kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani utaotekelezwa kupitia sekta tisa (9) za mageuzi (ii) kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii (iii) Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi (iv) vichocheo vya mageuzi na (v) Utawala, Amani, Usalama na Utulivu.

### (i) Kujenga Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani Utakaotekelezwa Kupitia Sekta Tisa (9) za Mageuzi

Kwa mwaka 2026/27 Mpango utajielekeza kutekeleza miradi na programu za maendeleo ili kuimarisha maeneo matatu ambayo ni: uchumi jumla tulivu na unaotabirika; sera za bajeti endelevu; na sekta ya nje iliyohimilivu na mseto. Aidha, miradi na programu za maendeleo zitakazotekelezwa zimelenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha ushirikiano na nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa ili kukuza kidiplomasia ya uchumi; na kujenga misingi imara ya ukuaji wa Uchumi. Vilevile, Mpango umeweka kipaumbele cha kuchochea mageuzi ya sekta tisa (9) za kimageuzi ambazo ni kilimo (mazao, mifugo, uvuvi na misitu); viwanda na uzalisha; ujenzi, madini na uchimbaji wa mawe, mafuta na gesi, utalii, fedha, michezo na ubunifu, na milki kuu (ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi).

**(ii) Kuimarisha Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii**

Programu na miradi itakayotekelezwa katika eneo hili inalenga kuongeza uwekezaji wa kimkakati katika masuala ya elimu, afya, huduma za maji safi na salama ili kupata nguvukazi yenye afya, maarifa na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko. Uwekezaji huo utahusisha kufanya mageuzi kwenye utoaji wa huduma za kijamii na kuchochea sekta za uzalishaji na uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu. Vilevile, uwekezaji huo utawezesha maandalizi ya kundi rika mbili; kuboresha vituo vya ubunifu na umahiri ili kukuza ubunifu na ujasiriamali; kuboresha upatikanaji wa huduma ya usafi wa mazingira pamoja na maji safi na salama; kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya; kuimarisha na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma jumuishi za kinga ya jamii kwa wananchi wote; na kuleta maendeleo jumuishi vijijini.

**(iii) Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi**

Utekelezaji wa programu na miradi katika eneo hili umelenga kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mazingira na kuweka misingi endelevu katika sekta zote ili kuhakikisha usalama na ustawi wa ikolojia. Eneo hili litajumuisha ukuaji wa miji, uhifadhi wa misitu na bioanuwai, nishati jadidifu na kuboresha mifumo ya utoaji tahadhari mapema; kuongeza uzalishaji wa mazao ya kibiashara yenye ustahimilivu wa tabianchi kwa kupanua umwagiliaji, na kuongeza matumizi ya pembejeo bora; kuimarisha utunzaji wa mazingira kupitia usimamizi wa utekelezaji wa mkakati wa nishati safi ya kupikia pamoja na kuimarisha usimamizi wa biashara ya hewa ukaa; na ustawi wa maisha ya watu.

**(iv) Vichocheo vya Mageuzi**

Kipaumbele katika eneo hili ni programu na miradi inayolenga kuongeza ushindani kimataifa kwa kuongeza tija, uwezo wa uzalishaji pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa na huduma nchini; kuvutia uwekezaji wa kimkakati na kuchochea uzalishaji wa ajira zenye tija. Uwekezaji utajikita kwenye miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; barabara, reli, meli, bandari, viwanja vya ndege, mabomba ya mafuta na gesi; kutekeleza mfumo wa kitaifa wa ubunifu; na kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na TEHAMA pamoja na usalama wa mtandao ili kuchochea uchumi wa kidijitali.

**(v) Utawala, Amani, Usalama na Utulivu**

Utekelezaji wa programu na miradi katika eneo hili umelenga: Kuimarisha utawala bora na ufanisi katika sekta ya umma ili kuleta uwajibikaji, uwazi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma; kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za uchumi ili kuweka msingi thabiti wa utekelezaji wa Dira 2050; kufanya maboresho ya sera, sheria, kanuni na taratibu ili kuleta ulinganifu wa sera na sheria na mikakati ya kisekta; na kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha ulinzi wa mipaka, rasilimali na usalama wa raia na mali zao.

27. Maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2026/27 ni: kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; ulipaji wa mishahara na deni la Serikali; ukamilishaji wa miradi na programu za maendeleo zinazoendelea; na kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza katika miradi yenye tija itakayochochea ukuaji wa uchumi, kuongeza fursa za ajira na mapato kwa Serikali. Moja ya maeneo ya kimkakati ni kuendeleza miundombinu wezeshi katika Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZs & EPZs) ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi.

### 4.5. Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/27

28. Kwa kuzingatia sera za bajeti na mikakati ya kukusanya mapato pamoja na udhibiti wa matumzi, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni 62,334.2 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la asilimia 10.3 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/26. Ukomo huu umefikiwa baada ya kuzingatia vigezo kadhaa vya msingi ikiwemo mwenendo halisi wa mapato ya ndani, ukomo wa nakisi ya bajeti usiozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa kulingana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Africa (SADC), Ongezeko la deni la Taifa, gharama za mikopo na ongezeko la malipo ya mikopo, sambamba na mabadiliko ya sera za washirika wa maendeleo. Sehemu kubwa ya ongezeko hili itagharamia mishahara, malipo ya deni la Serikali, malimbikizo ya madai ya wakandarasi, michango ya Serikali katika mfuko wa pensheni, mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na fedha za Mifuko ambazo kwa pamoja zitatumia takribani asilimia 75 ya ongezeko la bajeti. Mapato yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 46,791.3 ambapo mapato ya kodi ni shilingi bilioni 36,989.3, mapato mengine ni shilingi bilioni 9,238.8 (ikiwemo mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya shilingi bilioni 1,966.2) na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 563.1. Aidha, makadirio ya mapato ya ndani (kodi na mengine) ni sawa na asilimia 74.2 ya bajeti ya mwaka 2026/27. Kwa kuzingatia malengo ya Dira 2050, Serikali itaendelea kutumia njia mbadala za kugharamia miradi na kuandaa miradi inayokopesheka ili sekta binafsi itumie fursa hiyo kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

29. Mwaka 2026/27, matumizi na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 54,498.6 bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali ikilinganishwa na shilingi bilioni 48,775.0 ya mwaka 2025/26, sawa na

ongezeko la asilimia 11.7. Kati ya kiasi hicho, stahiki za watumishi ikijumuisha michango ya pensheni ni shilingi bilioni 9,985.7, gharama za bidhaa na huduma shilingi bilioni 8,302.9, malipo ya riba ni shilingi bilioni 7,257.9, ruzuku shilingi bilioni 24,942.0, mafao na misaada ya kijamii shilingi bilioni 790.1, gharama nyingine shilingi bilioni 189.6 na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi bilioni 3,030.4.

30. Serikali itaendelea kugharamia nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa kwa kutumia mikopo kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali (2025/26 – 2027/28). Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali inakadiria kukopa wastani wa shilingi bilioni 15,242.9. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 15,542.9 kwa mwaka 2026/27. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya ndani ni shilingi bilioni 6,557.7, mikopo ya nje yenye masharti nafuu shilingi bilioni 6,554.8 na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 2,430.4. Vilevile, Serikali inakadiria kulipa shilingi bilioni 7,835.6 kwa ajii ya malipo ya mtaji kwa mikopo iliyoiva, hivyo, mikopo halisi ni shilingi bilioni 7,407.3. Baadhi ya maeneo yenye ongezeko kubwa la bajeti ni kama inavyoonekana katika **jedwali Na. 3**. Aidha, v**iambatisho Na. 1A na 1B** vinaonesha mapendekezo ya makadirio ya matumizi kwa mafungu mbalimbali.

**Jedwali Na.3: Baadhi ya Maeneo yenye ongezeko kubwa la bajeti (milioni)**

| | 2025/26 | 2026/27 | Ongezeko |
|---|---|---|---|
| **Bajeti** | **56,490,252.22** | **62,334,193.23** | **5,843,941.01** |
| | | | |
| Ugharamiaji wa deni | 14,219,350.70 | 15,093,461.60 | 874,110.90 |
| Mishahara | 13,174,240.00 | 14,088,142.29 | 913,902.29 |
| Mchango wa Serikali katika mfuko wa pensheni (CFS others) | 3,131,303.65 | 3,581,819.65 | 450,516.00 |
| Mapato ya Serikali za Mitaa | 1,680,506.76 | 1,966,193.19 | 285,686.43 |
| Fedha zinazokusanywa na TRA kwa niaba ya taasisi Direct transfer (Funds) | 0 | 1,843,129.52 | 1,843,129.52 |
| **Jumla** | **32,205,401.11** | **36,572,746.25** | **4,367,345.14** |
| **Tofauti kati ya ongezeko la bajeti na ongezeko la matumizi yasio ingia katika mgawanyo** | | | **1,476,595.86** |

*Chanzo: Wizara ya Fedha*

31. Mfumo na ukomo wa bajeti kwa mwaka 2026/27 ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Mapendekezo ya Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27**

(shilingi milioni)

| | 2025/26 | | 2026/27 | |
|---|---|---|---|---|
| | Bajeti Iliyoidhinishwa | Bajeti iliyoboreshwa | 2026/27 Bajeti Inayopendekezwa | Ongezezo |
| **A: Mapato** | **41,536,016** | **41,391,220** | **46,791,299** | **13.0%** |
| Mapato ya kodi | 32,306,123 | 32,306,123 | 36,989,320 | **14.5%** |
| Misaada/Michango | 1,069,884 | 925,088 | 563,139 | **-39.1%** |
| Mapato mengine | 8,160,009 | 8,160,009 | 9,238,839 | **13.2%** |
| o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,680,507 | 1,680,507 | 1,966,193 | **17.0%** |
| | | | | |
| **B: Matumizi** | **45,994,829** | **45,994,829** | **51,468,233** | **11.9%** |
| **Mishahara na stahiki za watumishi** | **7,711,867** | **7,711,867** | **9,985,742** | **29.5%** |
| o/w Mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu | 4,754,850 | 4,754,850 | 5,324,212 | **12.0%** |
| Michango ya hifadhi za jamii | 2,240,141 | 2,240,141 | 2,569,421 | **14.7%** |
| **Gharama za bidhaa na huduma** | **7,812,245** | **7,812,245** | **8,302,857** | **6.3%** |
| o/w Malipo ya madeni ya watumishi, wazabuni na wakandara | 700,000 | 700,000 | 800,000 | **14.3%** |
| **Malipo ya riba** | **6,493,715** | **6,493,715** | **7,257,876** | **11.8%** |
| Malipo ya riba nje | 2,796,427 | 2,796,427 | 3,000,302 | **7.3%** |
| Malipo ya riba ndani kwa taasisi zisizo Serikali Kuu | 3,697,288 | 3,697,288 | 4,257,574 | **15.2%** |
| Malipo kwa taasisi ambazo ni Serikali Kuu | - | - | | |
| **Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji** | **1,936,023** | **1,936,023** | **2,032,825** | **5.0%** |
| Kwa mashirikia ya umma | 1,889,293 | 1,889,293 | 1,983,758 | **5.0%** |
| Kwa sekta nyingine | 46,730 | 46,730 | 49,067 | **5.0%** |
| **Ruzuku na michango** | **21,107,935** | **21,107,935** | **22,909,238** | **8.5%** |
| Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa | 9,703,349 | 9,703,349 | 10,412,288 | **7.3%** |
| o/w Mishahara ya watumishi | 6,162,616 | 6,162,616 | 6,470,747 | **5.0%** |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 1,793,891 | 1,793,891 | 1,883,585 | **5.0%** |
| Kwa taasisi za umma | 11,404,586 | 11,404,586 | 12,496,950 | **9.6%** |
| o/w Mishahara ya watumishi | 2,183,984 | 2,183,984 | 2,293,183 | **5.0%** |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 6,819,691 | 6,819,691 | 7,160,676 | **5.0%** |
| **Mafao na misaada ya kijamii** | **752,516** | **752,516** | **790,141** | **5.0%** |
| Mafao ya hifadhi za jamii | - | - | | |
| Misaada ya huduma za jamii | 10,473 | 10,473 | 10,997 | **5.0%** |
| Mafao na viinua mgongo | 742,042 | 742,042 | 779,144 | **5.0%** |
| **Gharama nyingine** | **180,528** | **180,528** | **189,554** | **5.0%** |
| | | | | |
| **Salio la Mapato na Matumizi** | **(4,458,813)** | **(4,603,609)** | **(4,676,935)** | **1.6%** |
| | | | | |
| **C: Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha** | **2,780,160** | **2,780,160** | **3,030,375** | **9.0%** |
| Gharama za majengo, miundombinu, mashine n.k | 2,666,037 | 2,666,037 | 2,905,980 | **9.0%** |
| Mali zisizozalishwa/mali za asili | 114,123 | 114,123 | 124,394 | **9.0%** |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti bila Misaada** | **(8,308,858)** | **(8,308,858)** | **(8,270,449)** | **-0.5%** |
| | | | | |
| **Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada** | **(7,238,973)** | **(7,383,770)** | **(7,707,309)** | **4.4%** |
| | | | | |
| **Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti** | 7,238,973 | 7,383,770 | 7,707,309 | **4.4%** |
| **Mikopo halisi** | **7,238,973** | **7,383,770** | **7,707,309** | **4.4%** |
| **D: Mikopo ya ndani** | **2,952,630** | **2,214,112** | **3,272,349** | **47.8%** |
| D1 - Mikopo ya ndani | 6,278,186 | 5,539,668 | 6,557,744 | **18.4%** |
| D2 - Malipo ya mikopo ya ndani | (3,325,557) | (3,325,557) | (3,285,395) | **-1.2%** |
| | | | | |
| **E: Mikopo ya nje** | **4,286,343** | **5,169,658** | **4,434,960** | **-14.2%** |
| E1 - Mikopo ya nje | 8,676,050 | 9,559,364 | 8,985,150 | **-6.0%** |
| o/w Mikopo ya Kibiashara | 2,629,012 | 2,629,012 | 2,430,372 | **-7.6%** |
| E2 - Malipo ya mikopo ya nje | (4,389,707) | (4,389,707) | (4,550,190) | **3.7%** |
| | | | | |
| **Jumla ya Bajeti ( A + D1 + E1)** | **56,490,252** | **56,490,252** | **62,334,193** | **10.3%** |
| **Nakisi ya bajeti/Pato la Taifa** | **-3.0%** | **-3.0%** | **-2.9%** | |
| | | | | |
| **Memo Items** | | | | |
| Pato la Taifa | 242,071,490 | 244,548,703 | 269,855,032 | |

***Chanzo**: Wizara ya Fedha*

### 4.6. Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti

32. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/27 unaweza kuathiriwa na vihatarishi ambavyo vitasababisha kutofikiwa kwa malengo ya kibajeti yaliyokusudiwa. Vihatarishi hivyo vimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni vihatarishi vya uchumi jumla na vihatarishi mahsusi.

#### 4.6.1. Vihatarishi vya Uchumi Jumla

33. Vihatarishi vya uchumi jumla vinaweza kutokea kutokana na sababu za asili na zisizo za asili za ndani na nje ya nchi. Baadhi ya vihatarishi vinavyoweza kuathiri viashiria vya uchumi jumla ni pamoja na mabadiliko ya viwango vya riba za mikopo, mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma, kushuka kwa thamani ya shilingi pamoja na mabadiliko ya sera za nje.

(i) **Mabadiliko ya Viwango vya Riba za Mikopo**

34. Viwango vya riba katika soko la fedha hupangwa kulingana na nguvu ya uhitaji na ugavi wa huduma za fedha, hususan mikopo. Kuongezeka kwa uhitaji wa mikopo ikilinganishwa na ugavi husababisha ongezeko la viwango vya riba katika sekta ya fedha. Ongezeko la viwango vya riba huongeza gharama za mikopo kwa sekta ya umma na sekta binafsi, kupungua kwa uwezo wa taasisi katika utekelezaji wa miradi na huduma kwa jamii, kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na ugavi wa bidhaa na huduma, kuongezeka kwa gharama za urejeshaji wa mikopo iliyoiva, kupungua kwa kasi ya uwekezaji katika sekta ya umma na binafsi, kuchochea mfumuko wa bei ya bidhaa na huduma, kupungua kwa mapato binafsi, mashirika, kampuni na Serikali, na kupungua kwa bei ya hisa katika soko la hisa. Athari hizi kwa pamoja zinaweza kusababisha mtikisiko wa hali ya kiuchumi, hususan kupungua kwa kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa.

35. Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na: Kuendelea kutekeleza na kusimamia kwa uthabiti sera ya fedha na bajeti ili kufikia malengo na shabaha za uchumi jumla; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ili kuvutia mitaji kutoka nje; kuendeleza soko la ndani la fedha; kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa na huduma za ndani; na kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134 na Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/18-2029/30.

(ii) **Mabadiliko ya Bei za Bidhaa**

36. Kushuka kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia, hususan madini na mazao ya kilimo ni matokeo ya tofauti ya nguvu ya uhitaji na ugavi wa bidhaa. Hali hii inaweza kutokea kutokana na matukio ya kivita, ukame, mafuriko, milipuko ya magonjwa, na migogoro wa kibiashara na kisiasa. Kushuka kwa bei ya bidhaa kunaweza kupunguza mapato yatokanayo na mauzo nje ya nchi na kuathiri uzalishaji wa mazao husika hapa nchini. Aidha, kupanda kwa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia, hususan bidhaa za petroli na mbolea kunaweza kuongeza matumizi ya fedha za kigeni katika kugharamia bidhaa hizo, kuongeza gharama za uzalishaji na ugavi wa bidhaa mbalimbali na uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Vilevile, hali hii itapunguza kasi ya uzalishaji wa mazao, kuongeza nakisi ya bajeti, upungufu wa fedha za kigeni, na kuongeza mfumuko wa bei nchini.

37. Hatua za kukabaliana na vihatarishi vya mabadiliko ya bei za bidhaa ni pamoja na kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, kuendelea kuwekeza kwenye uzalishaji wa nishati mbadala wa petroli kama vile gesi na umeme ili kupunguza athari za kupanda kwa bei ya bidhaa za petroli katika soko la dunia na kuwekeza kwenye miradi ya umwagiliaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira ili kuhakikisha shughuli za kilimo zinafanyika vipindi vyote vya mwaka. Pia, kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa, mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na teknolojia za kuhifadhi chakula, na kuongezea thamani za bidhaa.

(iii) **Kushuka kwa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

38. Thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni inategemea mzunguko wa fedha za kigeni, mizania ya biashara, sera za fedha na matarajio ya wawekezaji. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kunaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti kwa kuongeza matumizi hususan ugharamiaji wa deni la Serikali la nje na ununuzi na usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

39. Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa fedha za Kigeni, kuimarisha mifumo ya usimamizi wa sekta zinazochangia upatikanaji wa fedha za kigeni ikiwemo utalii, madini na kilimo, kuimarisha mifumo rasmi ya mauzo ya bidhaa na huduma nje, na kupunguza vikwazo vya kibiashara mipakani.

(iv) **Mabadiliko ya Sera za Nchi Wahisani**

40. Mabadiliko ya sera za nchi wahisani hutokea kutokana na mdororo wa shughuli za kiuchumi pamoja na mabadiliko ya uongozi wa kisiasa na mifumo ya uzalishaji wa bidhaa na huduma. Aidha, mabadiliko ya sera za nchi wahisani yanaweza kuathiri upatikanaji wa fedha za kigeni, misaada na mikopo inayotegemewa katika utekelezaji wa mpango na bajeti. Hali hii inaweza kuathiri uhusiano wa kidiplomasia, utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo, biashara, uwekezaji, utoaji wa huduma za kijamii, na ukuaji wa uchumi.

41. Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na: Kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya ndani; kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarisha shughuli za utafiti na ubunifu; kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia kwa kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/18-2029/30 na Sera ya Mambo ya Nje ya 2021 (Toleo la mwaka 2024).

**4.6.2. Vihatarishi Mahsusi**

42. Vihatarishi mahsusi ni pamoja na madeni sanjari, mabadiliko ya tabianchi na majanga, migogoro ya kisiasa na mahusiano ya kidiplomasia na shambulio la mifumo ya TEHAMA.

(i) **Madeni Sanjari**

43. Madeni sanjari hutokea pale ambapo Serikali na taasisi zake hazijatekeleza ipasavyo mikataba baina yake na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi. Kushindwa kutekeleza matakwa ya mikataba kunaweza kusababisha Serikali kugharamia malipo ya fidia na madai yatokanayo na amri za mahakama pamoja na taasisi za usuluhishi wa migogoro ya kibiashara. Aidha, Serikali inaweza ikabeba vihatarishi vya miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi iwapo itashindwa kutekeleza kikamilifu mikataba hiyo. Mazingira hayo yakijitokeza yanaweza kusababisha ongezeko la mzigo wa kibajeti kwa ajili ya kugharamia madai na deni la Serikali, hivyo kupunguza uwezo wa Serikali kugharamia mahitaji mengine hususan miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za kawaida.

44. Hatua za kukabiliana na vihatarishi vya madeni sanjari ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 na Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103, kuimarisha mifumo na taasisi za usimamizi wa mikataba, kuendelea kujenga uwezo katika usimamizi wa mikataba, na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa mikataba. Aidha, ni muhimu taasisi ziibue miradi inayokopesheka (Bankable projects) na kurejesha mikopo hiyo kwa kutumia mizania zao (balance sheet) ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa deni kama inavyofanyika kwenye baadhi ya taasisi kama TPA, Tanga UWASA na TANESCO.

(ii) **Mabadiliko ya Tabianchi na Majanga**

45. Mabadiliko ya tabianchi na majanga yanasababishwa na shughuli za kibinadamu na mifumo asili ya mazingira. Majanga yanayoweza kujitokeza ni kama vile tetemeko la ardhi, mlipuko wa volkano, mlipuko wa magonjwa, baa la njaa, ukame, wadudu waharibifu wa mazao, matukio ya moto na maporomoko ya ardhi. Aidha, mabadiliko ya tabianchi yanaweza kusababisha mafuriko, uhaba wa mvua, vimbunga na kuongezeka kwa kiwango cha joto. Kutokea kwa mabadiliko ya tabianchi na majanga kunaweza kusababisha vifo, kudorora kwa shughuli za uchumi, uharibifu wa miundombinu, mali na mifumo ya ikolojia. Hivyo, Serikali itahitaji bajeti ya dharura kwa ajili ya kutoa msaada kwa wahanga na urejeshaji wa miundombinu iliyoharibika.

46. Hatua za kukabiliana na vihatarishi hivi ni pamoja na: Kuimarisha Mfuko wa Dharura wa Taifa; kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032); kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 – 2027; kuimarisha mfumo wa uandaaji wa miradi kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma pamoja na maboresho yake kuhusu mabadiliko ya tabianchi na mazingira; na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati safi ya Kupikia (2024 – 2034). Hatua nyingine ni kuendelea kuwekeza katika miradi ya uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira, ujenzi wa mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji ya mvua, miradi ya umwagiliaji, matumizi ya mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na wadudu waharibifu na teknolojia za kuhifadhi chakula.

### (iii) Migogoro ya Kisiasa na Mahusiano ya Kidiplomasia

47. Migogoro ya kisiasa na mahusiano duni ya kidiplomasia ni matokeo ya mambo mbalimbali ikiwemo ushindani usio sawa wa kibiashara; ukiukaji wa misingi ya utawala bora na utawala wa sheria; ukosefu wa rasilimali; uchu wa madaraka; ukosefu wa ajira; na mabadiliko ya kisera na itikadi za kisiasa. Migogoro ya kisiasa ya ndani na nje ya nchi pamoja na kutetereka kwa mahusiano ya kidiplomasia kunaweza kuvuruga au kudumaza shughuli za kiuchumi na kijamii, na hivyo kuathiri upatikanaji wa mapato ya Serikali, kampuni, mashirika na watu binafsi; kupungua kwa misaada, mikopo na uwekezaji kutoka nje; kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji, uhitaji na ugavi wa mazao, bidhaa na huduma; na kuongezeka kwa mahitaji ya ziada ya ulinzi na usalama.

48. Hatua za kukabiliana na vihatarishi hivyo ni pamoja na kuendelea kuimarisha mifumo ya utawala bora na utawala wa sheria; kuimarisha mifumo na taasisi za usimamizi wa ushindani wa kibiashara; kudumisha na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kupitia mikataba ya ushirikiano na kidiplomasia; kuzalisha ajira stahiki na zenye staha; kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/18 – 2029/30 pamoja na Sera ya Mambo ya Nje ya 2021 (Toleo la mwaka 2024).

### (iv) Shambulio la Mifumo ya TEHAMA

49. Shambulio la mifumo linasababishwa na tabia ovu ya baadhi ya watu na taasisi, tamaa, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ukosefu wa ajira, na kasi ya mabadiliko ya teknolojia. Shambulio la mifumo ya TEHAMA linaweza kusababisha hasara za kifedha kutokana na uchepushaji wa mapato na matumizi ya Serikali na kuathiri utekelezaji wa bajeti. Aidha, shambulio la mifumo linaweza kudhoofisha upatikanaji wa huduma, uvujaji wa taarifa na kuchafua taswira ya Serikali.

50. Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na: Kuimarisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria; kuimarisha misingi ya uadilifu katika jamii; kuendelea kujenga uwezo na kuimarisha usalama wa mtandao wa Serikali; kutoa mafunzo endelevu kwa watumishi wa umma kuhusu utambuzi na namna ya kukabiliana na mashambulizi ya mtandao; kuongeza kasi ya uzalishaji wa ajira; utekelezaji wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya 2015; utekelezaji wa Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya 2015 na Sheria ya Serikali Mtandao ya 2019. Hatua nyingine ni pamoja na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Mtandao 2024 – 2029 na Mkakati wa Ulinzi wa Kimtandao Serikalini wa Mwaka 2022–2027.

### (v) Kihatarishi cha Kiutendaji

51. Ufanisi mdogo katika utekelezaji wa mpango na bajeti ni kihatarishi cha kiutendaji (operational risk) kinachojitokeza pale ambapo taasisi au Serikali inashindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa wakati, kwa ubora, na kwa gharama zilizokadiriwa. Hali hii husababishwa na udhaifu wa ndani wa mifumo ya usimamizi, hususan usimamizi wa mikataba, ukosefu wa rasilimali fedha na watu

wenye ujuzi, pamoja na uratibu hafifu miongoni mwa taasisi zinazohusika katika utekelezaji wa mpango na bajeti. Aidha, mabadiliko ya mara kwa mara ya kisera na kiutawala, urasimu katika maamuzi, kuweka malengo yasiyoendana na uhalisia, rushwa, na ukosefu wa uwazi na uwajibikaji huongeza uwezekano wa mpango na bajeti kutotekelezwa kwa ufanisi. Matokeo yake ni kuchelewa kwa miradi ya maendeleo, miradi na huduma kukosa thamani halisi ya fedha, kushuka kwa tija ya shughuli za kiuchumi, utegemezi wa kibajeti, na kupungua kwa imani ya wadau kwa taasisi za umma.

52. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi kwa kutumia mbinu shirikishi na teknolojia za kidijitali, kujenga uwezo wa watumishi katika usimamizi wa fedha na utendaji, kuimarisha uwazi na uwajibikaji, kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya umma yenye sifa za kibiashara, na kuhakikisha mawanda ya shughuli za umma katika mpango na bajeti yanazingatia uhalisia wa mapato na mazingira ya utekelezaji wake.

## 5.0. HITIMISHO

53. Katika mwaka 2026/27, Serikali inatarajia kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo Mkakati wa Muda wa Kati wa Kuongeza Mapato 2025/26 – 2027/28 ili kuongeza wigo wa kodi na hivyo kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kupunguza utegemezi wa kibajeti. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia na kudhibiti matumizi kwa kuyawianisha na hali halisi ya upatikanaji wa mapato na kutoa kipaumbele kwa mahitaji yasiyoepukika ikiwemo ugharamiaji wa mishahara, deni la Serikali, hati za madai na huduma za jamii. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa na kuweka kipaumbele kwa miradi inayoendelea.

**Kiambatisho 1A: MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, OFISI ZA WAKUU WA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2026/27 (Shilingi Milioni)**

| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti Iliyoidhinishwa (Matumizi Mengineyo - OC) 2025/26 | Mapendekezo ya Bajeti (Matumizi Mengineyo - OC) 2026/27 |
|---|---|---|---|
| | **A: MFUKO MKUU WA SERIKALI** | | |
| 001 | Deni la Serikali (Riba na Mtaji) | 14,219,350.7 | 15,117,796.6 |
| 022 | Mfuko Mkuu wa Huduma | 3,131,303.6 | 3,581,819.7 |
| | **Jumla Ndogo (A)** | **17,350,654.4** | **18,699,616.2** |
| | | | |
| | **B: WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI** | | |
| 002 | Tume ya Utumishi wa Walimu | 8,110.3 | 8,110.3 |
| 003 | Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi | 3,475.4 | 3,127.9 |
| 004 | Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 3,283.4 | 2,955.1 |
| 005 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 65,148.8 | 65,148.8 |
| 006 | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | 11,430.4 | 10,287.4 |
| 007 | Msajili wa Hazina | 51,922.2 | 51,922.2 |
| 010 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 4,164.5 | 4,164.5 |
| 011 | Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji | 13,675.4 | 13,675.4 |
| 012 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 5,841.7 | 5,841.7 |
| 013 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | 5,162.4 | 5,162.4 |
| 014 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | 31,186.3 | 31,186.3 |
| 015 | Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 4,313.4 | 3,882.0 |
| 016 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 35,481.4 | 35,481.4 |
| 018 | Tume ya Elimu na Sayansi | 1,702.2 | 1,532.0 |
| 019 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 33,717.8 | 33,717.8 |
| 020 | Ofisi ya Rais - Ikulu | 23,409.5 | 23,409.5 |
| 021 | Hazina | 783,658.9 | 705,560.4 |
| 023 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 91,566.3 | 52,709.7 |
| 024 | Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika | 9,033.6 | 8,130.2 |
| 025 | Waziri Mkuu (Ofisi Binafsi) | 28,116.7 | 28,116.7 |
| 026 | Makamu wa Rais (Ofisi Binafsi) | 18,879.5 | 18,879.5 |
| 027 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 30,015.7 | 21,614.2 |
| 028 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Jeshi la Polisi | 446,306.6 | 398,034.7 |
| 029 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Magereza | 123,398.8 | 115,850.4 |
| 030 | Ofisi ya Rais - IKULU | 1,013,317.2 | 1,013,317.2 |
| 031 | Ofisi ya Makamu wa Rais | 17,950.6 | 16,155.6 |
| 032 | Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala | 36,668.3 | 36,668.3 |
| 033 | Sekretarieti ya Maadili | 9,966.7 | 8,970.0 |
| 034 | Wizara ya Mammbo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 273,661.5 | 273,661.5 |

| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti Iliyoidhinishwa (Matumizi Mengineyo - OC) 2025/26 | Mapendekezo ya Bajeti (Matumizi Mengineyo - OC) 2026/27 |
|---|---|---|---|
| | **B: WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI** | | |
| 035 | Ofisi ya Mwendesha Mashataka wa Serikali | 109,671.7 | 109,671.7 |
| 037 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 34,594.1 | 36,680.2 |
| 038 | Wizara ya Ulinzi (Ng'ome) | 532,275.9 | 532,275.9 |
| 039 | Jeshi la Kujenga Taifa | 160,224.1 | 160,224.1 |
| 040 | Mfuko wa Mahakama | 143,386.0 | 143,386.0 |
| 041 | Wizara ya Katiba na Sheria | 30,992.6 | 27,893.3 |
| 042 | Mfuko wa Bunge | 149,327.7 | 149,327.7 |
| 043 | Wizara ya Kilimo | 54,536.8 | 44,083.2 |
| 044 | Wizara ya Viwanda na Biashara | 18,081.3 | 16,273.2 |
| 045 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 87,357.0 | 87,357.0 |
| 046 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | 53,364.2 | 48,027.8 |
| 048 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 37,559.1 | 33,803.2 |
| 049 | Wizara ya Maji | 18,081.4 | 16,273.2 |
| 050 | Wizara ya Fedha | 80,571.8 | 72,514.6 |
| 051 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | 41,981.3 | 41,981.3 |
| 052 | Wizara ya Afya | 151,015.0 | 135,913.5 |
| 053 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | 26,469.5 | 23,822.6 |
| 055 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 8,291.4 | 8,291.4 |
| 056 | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 27,108.2 | 24,397.3 |
| 057 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 15,579.9 | 15,579.9 |
| 058 | Wizara ya Nishati | 69,932.3 | 52,939.1 |
| 059 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 5,627.2 | 5,627.2 |
| 061 | Tume ya Uchaguzi | 5,715.6 | 5,715.6 |
| 062 | Wizara ya Uchukuzi | 28,784.6 | 25,906.1 |
| 065 | Ofisi Ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano | 15,117.4 | 11,728.1 |
| 066 | Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango | 34,000.0 | 34,000.0 |
| 067 | Sekretarieti ya Ajira | 10,782.6 | 10,782.6 |
| 068 | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 7,527.0 | 6,774.3 |
| 069 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 123,523.3 | 111,171.0 |
| 091 | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya | 18,037.8 | 18,037.8 |
| 092 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania | 5,493.3 | 4,943.9 |
| 093 | Idara ya Uhamiaji | 58,830.2 | 58,830.2 |
| 094 | Tume ya Utumishi wa Umma | 6,862.3 | 6,862.3 |

| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti Iliyoidhinishwa (Matumizi Mengineyo - OC) 2025/26 | Mapendekezo ya Bajeti (Matumizi Mengineyo - OC) 2026/27 |
|---|---|---|---|
| | **B: WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI** | | |
| 096 | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo | 28,065.5 | 28,065.5 |
| 098 | Wizara ya Ujenzi | 5,439.7 | 4,895.7 |
| 099 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 54,251.9 | 48,826.7 |
| 100 | Wizara ya Madini | 76,110.8 | 76,110.8 |
| 101 | Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria | 16,454.2 | 16,454.2 |
| 104 | Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana | - | 25,876.3 |
| | **Jumla Ndogo (B)** | **5,535,590.4** | **5,278,597.7** |
| | | | |
| | **C: OFISI ZA WAKUU WA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA** | | |
| 036 | Katavi | 10,232.3 | 10,232.3 |
| 047 | Simiyu | 14,474.1 | 14,474.1 |
| 054 | Njombe | 17,388.1 | 17,388.1 |
| 063 | Geita | 15,061.0 | 15,061.0 |
| 070 | Arusha | 16,566.9 | 16,566.9 |
| 071 | Pwani | 22,777.9 | 22,777.9 |
| 072 | Dodoma | 18,470.6 | 18,470.6 |
| 073 | Iringa | 12,690.8 | 12,690.8 |
| 074 | Kigoma | 18,495.1 | 18,495.1 |
| 075 | Kilimanjaro | 18,003.4 | 18,003.4 |
| 076 | Lindi | 13,178.3 | 13,178.3 |
| 077 | Mara | 20,934.7 | 20,934.7 |
| 078 | Mbeya | 17,958.3 | 17,958.3 |
| 079 | Morogoro | 23,174.1 | 23,174.1 |
| 080 | Mtwara | 18,550.1 | 18,550.1 |
| 081 | Mwanza | 20,691.7 | 20,691.7 |
| 082 | Ruvuma | 18,261.5 | 18,261.5 |
| 083 | Shinyanga | 13,721.8 | 13,721.8 |
| 084 | Singida | 16,915.7 | 16,915.7 |
| 085 | Tabora | 20,159.3 | 20,159.3 |
| 086 | Tanga | 25,705.2 | 25,705.2 |
| 087 | Kagera | 19,316.8 | 19,316.8 |
| 088 | Dar es Salaam | 10,636.5 | 10,636.5 |
| 089 | Rukwa | 11,218.4 | 11,218.4 |
| 090 | Songwe | 11,180.6 | 11,180.6 |
| 095 | Manyara | 15,536.1 | 15,536.1 |
| | **Jumla Ndogo (C )** | **441,299.3** | **441,299.3** |
| | | | |
| | **Makusanyo ya ndani ya Halmashauri (D)** | **1,067,065.3** | **1,238,701.7** |
| | | | |
| | **Mishahara ( E )** | **13,174,240.0** | **14,088,142.3** |
| | | | |
| | **Jumla Kuu ya Matumizi ya Kawaida (A+B+C+D+E)** | **37,568,849.3** | **39,746,357.2** |

**Kiambatisho 1B**: **MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA MAENDELEO KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, OFISI ZA WAKUU WA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2026/27 (Shilingi Milioni)**

| A: WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti Iliyoidhinishwa kwa mwaka 2025/26 | | | Mapendekezo ya Bajeti ya Uwekezaji kwa mwaka 2026/27 | | |
| | | Uwekezaji wa Ndani | Misaada na Mikopo | Jumla | Uwekezaji wa Ndani | Misaada na Mikopo | Jumla |
| 002 | Tume ya Utumishi wa Walimu | 264.2 | 1,678.5 | 1,942.7 | 264.2 | 1,678.5 | 1,942.7 |
| 003 | Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi | 2,520.6 | - | 2,520.6 | 8,900.0 | - | 8,900.0 |
| 004 | Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 1,177.5 | - | 1,177.5 | 897.5 | - | 897.5 |
| 005 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 259,617.8 | 49,104.2 | 308,722.0 | 259,617.8 | 49,104.2 | 308,722.0 |
| 006 | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | 142.0 | 1,136.4 | 1,278.4 | 142.0 | 1,000.0 | 1,142.0 |
| 007 | Msajili wa Hazina | 370.7 | 1,300.0 | 1,670.7 | 370.7 | - | 370.7 |
| 010 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 958.9 | - | 958.9 | 958.9 | - | 958.9 |
| 011 | Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji | 6,182.7 | 6,292.6 | 12,475.3 | 6,182.7 | 2,958.7 | 9,141.4 |
| 014 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | 18,013.5 | - | 18,013.5 | 18,013.5 | - | 18,013.5 |
| 015 | Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 276.0 | - | 276.0 | 276.0 | - | 276.0 |
| 016 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 788.7 | - | 788.7 | 788.7 | - | 788.7 |
| 021 | Hazina | 588,912.0 | 101,824.5 | 690,736.4 | 1,667,912.0 | 217,320.6 | 1,885,232.6 |
| 023 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 741.4 | 4,090.1 | 4,831.5 | 741.4 | 3,000.0 | 3,741.4 |
| 024 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania | 697.2 | - | 697.2 | 697.2 | - | 697.2 |

| A: WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti Iliyoidhinishwa kwa mwaka 2025/26 | | | Mapendekezo ya Bajeti ya Uwekezaji kwa mwaka 2026/27 | | |
| | | Uwekezaji wa Ndani | Misaada na Mikopo | Jumla | Uwekezaji wa Ndani | Misaada na Mikopo | Jumla |
| 027 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 564.0 | - | 564.0 | 264.0 | - | 264.0 |
| 028 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Jeshi la Polisi | 202,755.0 | 600.0 | 203,355.0 | 202,755.0 | - | 202,755.0 |
| 029 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Magereza | 11,189.1 | 2,303.5 | 13,492.6 | 11,189.1 | - | 11,189.1 |
| 030 | Ofisi ya Rais - IKULU | 88,934.3 | 58,538.8 | 147,473.1 | 88,934.3 | 8,538.8 | 97,473.1 |
| 031 | Ofisi ya Makamu wa Rais | 4,602.0 | 14,457.6 | 19,059.6 | 4,602.0 | 24,134.7 | 28,736.7 |
| 032 | Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 19,755.5 | - | 19,755.5 | 19,755.5 | - | 19,755.5 |
| 033 | Sekretarieti ya Maadili | 3,000.0 | - | 3,000.0 | 3,000.0 | - | 3,000.0 |
| 034 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 45,540.0 | - | 45,540.0 | 45,540.0 | - | 45,540.0 |
| 035 | Ofisi ya Mwendesha Mashataka wa Serikali | 15,866.1 | - | 15,866.1 | 15,866.1 | - | 15,866.1 |
| 037 | Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu | 741.4 | 6,766.8 | 7,508.2 | 741.4 | 4,297.6 | 5,039.0 |
| 038 | Wizara ya Ulinzi (Ng'ome) | 48,867.6 | - | 48,867.6 | 48,867.6 | - | 48,867.6 |
| 039 | Jeshi la Kujenga Taifa | 9,929.9 | - | 9,929.9 | 9,929.9 | - | 9,929.9 |
| 040 | Mfuko wa Mahakama | 18,601.2 | 44,424.0 | 63,025.2 | 18,601.2 | 4,090.0 | 22,691.2 |
| 041 | Wizara ya Katiba na Sheria | 44,415.5 | 8,143.3 | 52,558.8 | 44,415.5 | 446.9 | 44,862.3 |
| 042 | Mfuko wa Bunge | 11,385.9 | 407.5 | 11,793.3 | 11,385.9 | 643.1 | 12,029.0 |

| A: WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti Iliyoidhinishwa kwa mwaka 2025/26 | | | Mapendekezo ya Bajeti ya Uwekezaji kwa mwaka 2026/27 | | |
| | | Uwekezaji wa Ndani | Misaada na Mikopo | Jumla | Uwekezaji wa Ndani | Misaada na Mikopo | Jumla |
| 043 | Wizara ya Kilimo | 424,328.0 | 227,947.9 | 652,275.9 | 360,678.8 | 206,666.9 | 567,345.7 |
| 044 | Wizara ya Viwanda na Biashara | 27,870.7 | 14,016.8 | 41,887.5 | 23,690.1 | - | 23,690.1 |
| 045 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 8,828.0 | 3,276.0 | 12,104.0 | 8,828.0 | 3,000.0 | 11,828.0 |
| 046 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | 1,186,988.0 | 950,476.2 | 2,137,464.2 | 1,333,177.0 | 267,736.1 | 1,600,913.1 |
| 048 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 5,732.5 | 56,325.4 | 62,057.8 | 5,732.5 | 65,902.5 | 71,635.0 |
| 049 | Wizara ya Maji | 340,463.7 | 484,033.2 | 824,496.9 | 401,203.7 | 671,938.0 | 1,073,141.7 |
| 050 | Wizara ya Fedha | 10,946.6 | 38,545.0 | 49,491.5 | 10,946.6 | 167,171.0 | 178,117.5 |
| 051 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | 79,067.9 | 23,626.1 | 102,694.0 | 79,067.9 | 35,893.6 | 114,961.5 |
| 052 | Wizara ya Afya | 789,458.6 | 347,649.5 | 1,137,108.1 | 789,458.6 | 358,566.6 | 1,148,025.2 |
| 053 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | 15,415.4 | 11,526.1 | 26,941.5 | 15,415.4 | 20,971.0 | 36,386.4 |
| 055 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | - | - | - | - | - | - |
| 056 | Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 717,316.9 | 400,350.2 | 1,117,667.1 | 878,242.4 | 376,529.2 | 1,254,771.6 |
| 057 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 260,000.0 | - | 260,000.0 | 500,000.0 | - | 500,000.0 |
| 058 | Wizara ya Nishati | 1,466,020.3 | 420,492.9 | 1,886,513.2 | 1,602,449.7 | 961,915.1 | 2,564,364.8 |
| 059 | Tume ya Kurekebisha Sheria | - | - | - | - | - | - |
| 061 | Tume Huru ya Uchaguzi | 367,617.8 | - | 367,617.8 | 18,380.9 | - | 18,380.9 |
| 062 | Wizara ya Uchukuzi | 2,452,512.4 | 168,533.6 | 2,621,046.1 | 2,452,512.4 | 294,184.4 | 2,746,696.8 |

| A: WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti Iliyoidhinishwa kwa mwaka 2025/26** | | | **Mapendekezo ya Bajeti ya Uwekezaji kwa mwaka 2026/27** | | |
| | | **Uwekezaji wa Ndani** | **Misaada na Mikopo** | **Jumla** | **Uwekezaji wa Ndani** | **Misaada na Mikopo** | **Jumla** |
| 065 | Ofisi Ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano | 12,812.4 | 509.7 | 13,322.1 | 11,812.4 | - | 11,812.4 |
| 066 | Tume ya Taifa ya Mipango | 8,000.0 | 1,361.3 | 9,361.3 | 8,000.0 | 1,319.5 | 9,319.5 |
| 067 | Sekretarieti ya Ajira | 1,408.8 | - | 1,408.8 | 1,000.0 | - | 1,000.0 |
| 068 | Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 98,480.9 | 178,566.6 | 277,047.5 | 98,480.9 | 110,962.4 | 209,443.3 |
| 069 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 32,476.1 | 49,810.5 | 82,286.5 | 23,134.8 | 39,166.7 | 62,301.4 |
| 091 | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya | 1,314.5 | - | 1,314.5 | 1,314.5 | - | 1,314.5 |
| 092 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania | 5,280.0 | 15,588.0 | 20,868.0 | - | 4,908.3 | 4,908.3 |
| 093 | Idara ya Uhamiaji | 77,585.2 | - | 77,585.2 | 77,585.2 | - | 77,585.2 |
| 094 | Tume ya Utumishi wa Umma | 500.2 | - | 500.2 | 500.2 | - | 500.2 |
| 096 | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo | 458,190.8 | - | 458,190.8 | 458,190.8 | - | 458,190.8 |
| 098 | Wizara ya Ujenzi | 1,209,223.1 | 603,967.8 | 1,813,190.9 | 1,544,872.1 | 1,012,464.3 | 2,557,336.5 |
| 099 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 227,994.4 | 147,144.0 | 375,138.4 | 193,795.2 | 141,304.5 | 335,099.7 |
| 100 | Wizara ya Madini | 71,507.7 | 53,097.1 | 124,604.8 | 71,507.7 | - | 71,507.7 |
| 104 | Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana | - | - | - | 1,000.0 | 853.0 | 1,853.0 |
| | **Jumla Ndogo (A)** | **11,764,151.6** | **4,497,911.5** | **16,262,063.1** | **13,462,588.1** | **5,058,666.1** | **18,521,254.1** |

| B: OFISI ZA WAKUU WA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti Iliyoidhinishwa kwa mwaka 2025/26** | | | **Mapendekezo ya Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka 2026/27** | | |
| | | **Uwekezaji wa Ndani** | **Misaada na Mikopo** | **Jumla** | **Uwekezaji wa Ndani** | **Misaada na Mikopo** | **Jumla** |
| 036 | Katavi | 21,618.5 | 19,201.0 | 40,819.5 | 21,618.5 | 7,076.0 | 28,694.4 |
| 047 | Simiyu | 34,586.0 | 26,606.1 | 61,192.1 | 34,586.0 | 10,898.2 | 45,484.2 |
| 054 | Njombe | 34,161.6 | 24,706.4 | 58,867.9 | 34,161.6 | 5,576.3 | 39,737.9 |
| 063 | Geita | 44,298.6 | 31,697.9 | 75,996.5 | 44,298.6 | 12,992.6 | 57,291.2 |
| 070 | Arusha | 72,662.6 | 29,341.7 | 102,004.3 | 72,662.6 | 10,986.2 | 83,648.8 |
| 071 | Pwani | 55,474.2 | 36,847.4 | 92,321.6 | 55,474.2 | 10,846.7 | 66,320.9 |
| 072 | Dodoma | 52,195.6 | 37,949.2 | 90,144.8 | 52,195.6 | 21,004.2 | 73,199.8 |
| 073 | Iringa | 35,094.5 | 28,938.2 | 64,032.7 | 35,094.5 | 7,473.0 | 42,567.5 |
| 074 | Kigoma | 44,332.6 | 42,562.6 | 86,895.2 | 44,332.6 | 10,585.8 | 54,918.3 |
| 075 | Kilimanjaro | 55,367.0 | 26,695.7 | 82,062.7 | 55,367.0 | 7,631.0 | 62,998.0 |
| 076 | Lindi | 32,890.7 | 25,979.3 | 58,870.0 | 32,890.7 | 8,449.5 | 41,340.2 |
| 077 | Mara | 52,172.6 | 35,411.6 | 87,584.2 | 52,172.6 | 9,467.6 | 61,640.2 |
| 078 | Mbeya | 45,302.1 | 34,851.5 | 80,153.6 | 45,302.1 | 10,448.8 | 55,750.9 |
| 079 | Morogoro | 56,284.2 | 43,026.3 | 99,310.6 | 56,284.2 | 12,344.6 | 68,628.8 |
| 080 | Mtwara | 38,819.9 | 35,610.2 | 74,430.1 | 38,819.9 | 8,520.1 | 47,340.0 |
| 081 | Mwanza | 65,794.4 | 49,759.0 | 115,553.4 | 65,794.4 | 14,718.6 | 80,513.0 |
| 082 | Ruvuma | 42,678.3 | 34,463.7 | 77,141.9 | 42,678.3 | 7,439.3 | 50,117.5 |
| 083 | Shinyanga | 31,979.1 | 28,557.5 | 60,536.6 | 31,979.1 | 10,036.7 | 42,015.8 |
| 084 | Singida | 41,308.6 | 29,046.6 | 70,355.2 | 41,308.6 | 10,708.8 | 52,017.4 |
| 085 | Tabora | 50,744.1 | 45,884.9 | 96,629.1 | 50,744.1 | 14,568.4 | 65,312.5 |
| 086 | Tanga | 60,702.2 | 54,096.1 | 114,798.3 | 60,702.2 | 11,491.7 | 72,193.9 |
| 087 | Kagera | 59,550.1 | 40,464.4 | 100,014.6 | 59,550.1 | 13,128.4 | 72,678.5 |
| 088 | Dar es Salaam | 46,290.3 | 43,914.0 | 90,204.3 | 46,290.3 | 14,646.7 | 60,936.9 |
| 089 | Rukwa | 25,035.2 | 18,865.6 | 43,900.7 | 25,035.2 | 5,728.0 | 30,763.2 |
| 090 | Songwe | 28,060.6 | 27,146.1 | 55,206.7 | 28,060.6 | 4,597.0 | 32,657.7 |
| 095 | Manyara | 40,505.2 | 26,370.6 | 66,875.8 | 40,505.2 | 10,145.1 | 50,650.3 |
| | **Jumla Ndogo (B )** | **1,167,908.9** | **877,993.5** | **2,045,902.3** | **1,167,908.9** | **271,509.1** | **1,439,417.9** |
| | | | | | | | |
| | **Elimu Msingi Bila Malipo** | **510,968.5** | **-** | **510,968.5** | **56,543.0** | **-** | **56,543.0** |
| | | | | | | | |
| | **Makusanyo ya Halmashauri ( C)** | **613,441.4** | **-** | **613,441.4** | **727,491.5** | **-** | **727,491.5** |
| | | | | | | | |
| | **Jumla Kuu (A+B+C)** | **13,545,501.9** | **5,375,904.9** | **18,921,406.9** | **15,414,531.4** | **5,330,175.1** | **20,744,706.5** |

**Tanbihi**: Kiasi cha shilingi bilioni 1,843.1 hakijagawanywa katika mafungu kwa kuwa ni makusanyo ya TRA yanayopelekwa moja kwa moja kwenye mifuko ikiwemo: shilingi bilioni 64.0 Mfuko wa UKIMWI, shilingi bilioni 193.5 Bima ya Afya kwa Wote, shilingi bilioni 284.5 Bodi ya Korosho, shilingi bilioni 532.7 Shirika la Hifadhi za Taifa (asilimia 60 ya mapato), shilingi bilioni 249.7 Hifadhi ya Ngorongoro (asilimia 60 ya mapato), shilingi bilioni 372.8 Mfuko wa Dharura na shilingi bilioni 145.9 mapato ya *Customs Processing Fees* yanayobaki TRA.